الرد على الأحباش

ar-Radd ´alaa al-Ahbaash

Mwandishi:
Imaam Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy

Mfasiri:
Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

Swali – Maneno ya Ahbaash kuhusu Allaah 3

Jibu – Imani ya Ahbaash 4

Utangulizi 4

Tofauti kati ya mwanachuoni na mjinga 6

Aina mbili ya wanachuoni 7

Maneno ya haki yanayokusudiwa ndani yake batili 9

Makundi mawili yanayomnasibishia Allaah kuwa na mahali 12

Mjakazi – Allaah Yuko wapi? 17

Mkono wa Allaah 24

Swali – Maneno ya Ahbaash kuhusu Allaah

Shaykh wetu, baadhi ya Ahbaash ambao ni wanafuzni wa ´Abdullaah al-Habashiy wamejadiliana na baadhi ya wanawake wa nchi hii kwa njia ya kiakili. Wanazungumza nao kwa mfano wa njia ya kusema:

”Ni nani kaumba mahali”?

Wanawake wanajibu:

”Allaah.”

Hivyo Habashiy huyu anasema:

”Je, inajuzu kwa Allaah ambaye ndiye Ameumba mahali awe katika mahapa hapo?”

Mwanamke huyo anajibu:

”Hapana.”

Anafika anasema:

”Kwa hiyo Allaah hakuna kinachomuwekea mpaka, Hayuko juu na chini, wala mbele na nyuma, wala kuliani na kushotoni. Kadhalika sifa nyenginezo zote.”

Anasema:

”Mkono unaojulikana ni mkono ule ulio na mwanaadamu. Je, inajuzu kwa Muumba kuwa na kitu cha mwanaadamu, wakati Yeye ndiye Muumbaji wa viumbe”?

Tupe faida Allaah Akujaze kheri.

Jibu – Imani ya Ahbaash

Utangulizi

Imaam al-Albaaniy anajibu:

Himdi zote zinamstahikia Allaah. Tunamhimidi Yeye, tunamuomba kinga na tunamuomba msamaha. Tunajilinda Kwake kutokamana na shari ya nafsi zetu na uovu wa matendo yetu. Anayeongozwa na Allaah, basi hakuna wa kumpoteza. Anayepotezwa na Allaah, basi hakuna wa kumwongoza. Ninashuhudia ya kwamba hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah, hali ya kuwa ni Mmoja pekee asiyekuwa na mshirika. Ninashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja na ni Mtume Wake.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ

“Enyi walioamini! Mcheni Allaah kama apasavyo kuogopwa na wala msife isipokuwa nyinyi ni waislamu.”[1]

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni kutokana na nafsi moja na akaumba kutoka humo mke wake na akaeneza kutoka hao wawili wanaume wengi na wanawake. Na mcheni Allaah ambaye Kwake mnaombana na jamaa. Hakika Allaah amekuwa juu yenu ni Mwenye kuchunga.”[2]

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا

“Enyi mlaomini! Mcheni Allaah na semeni kauli ya kweli. Atakutengenezeeni matendo yenu na atakusameheni madhambi yenu; na

[1] 03:102

[2] 04:01

anayemtii Allaah na Mtume Wake, basi kwa hakika amefanikiwa mafaniko makubwa."[3]

Amma ba´d:

Hakika bora ya maneno ni Maneno ya Allaah. Uongofu bora ni uongofu wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Shari ya mambo ni mambo ya kuzua. Kila kinachozushwa ni Bid´ah. Kila Bid´ah ni upotevu. Kila upotevu ni Motoni.

Kabla ya kuanza kujibu swali hili ninataka kuwatuliza Waislamu wote, waliohudhuria na ambao hawakudhuhuria, wanaume na wanawake, ya kwamba Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) Ametakasika kutokamana na kila mahali. Hilo ni kwa sababu wakati mtu anapotaja neno "mahali" anakusudia ambapo hapakuwepo kisha baadaye Allaah (´Azza wa Jall) Akapaumba na Akafanya kupatikane mahali kwa viumbe wote hawa katika wanaadamu, majini na Malaika. Lakini neno ambalo watu hawa wanataja, na wanajulikana kwa wanachuoni kuwa ni wenye kuhuisha Sunnah mbaya wanayoitoa katika elimu ya falsafa iliyojengwa juu ya akili, lau akili hii ingelikuwa ni moja kwa watu wote, baina ya Waislamu na makafiri, wema na waovu. Laiti akili hii ingelikuwa ni akili moja ili iweze kuwa sahihi kwa kila alie na akili kurejea katika hukumu yake. Lakini akili ni yenye kutofautiana kwa kiasi kikubwa kwa watu wote. Kwa ajili hiyo huu ni upumbavu mkubwa kwa wale ambao wanajinasibisha na Uislamu, kwa Ikhlaasw au pasi na Ikhlaasw, hesabu yao iko kwa Allaah. Lau akili ingelikuwa moja, basi wangelikuwa na sababu chache ya kuhukumu kwa akili yao, lakini akili ni yenye kutofautiana – kama tulivyosema na sitaki kukariri kwa ufafanuzi – kati ya mwema na muovu.

[3] 33:70-71

Tofauti kati ya mwanachuoni na mjinga

Hivi sasa nitataja tofauti nyingine. Akili ya mwanachuoni inatofautiana sana na akili ya mjinga. Simaanishi akili ya msomi wa Shari´ah, bali ninachomaanisha ni akili ya msomi wa elimu yoyote ile. Akili hii inatofautiana sana na akili nyingine ambayo sio ya msomi wa elimu ya yule mtu mwenye akili ya elimu ya kwanza. Kwa mfano, tabibu mwenye akili hawezi akashirikiana katika akili na elimu yake na mtu ambaye hashirikiani naye katika kazi ya utabibu, na kinyume chake. Mtu ambaye kwa mfano ni msomi wa fizikia au kemia hawezi akamshirikisha mtu ambaye ni msomi wa kazi ya utabibu. Mwishoni tunasema ya kwamba, ni jambo lisilowezekana mwanachuoni aliye na ufahamu wa Qur-aan na Sunnah akawa kama mtu aliye na akili lakini ni mjinga wa Qur-aan na Sunnah. Mada hii ni muhimu kuliko mgawanyo na maelezo haya. Mwanachuoni aliye na ufahamu wa Qur-aan na Sunnah na kwa mujibu wa mfumo wa Salaf-us-Swaalih, akili yake haiwezi kuwa kama akili ya yule ambaye anaiegemeza akili yake katika kuifahamu Qur-aan na Sunnah na isitoshe ufahamu wake haurejeshi kwa yale waliyokuwemo Salaf-us-Swaalih.

Aina mbili ya wanachuoni

Kwa kumalizia mgawanyo huu, tuseme kuna wanachuoni wawili wa Qur-aan na Sunnah. Mmoja wao ufahamu wake anauegemeza katika Qur-aan na Sunnah juu ya mapokezi ya Salafiyyah, ambayo kwanza yanarudi kwa Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambao ndio wa kwanza waliotangulia, halafu waliowafuata kwa wema mpaka siku ya Qiyaamah. Huyu ambaye anategemea Qur-aan na Sunnah na juu ya mfumo wa Salaf, akili yake inatofautiana kwa kiasi kikubwa na yule mtu wa pili ambaye naye pia anategemea Qur-aan na Sunnah, lakini anaitegemeza akili yake katika kuvifahamu na sio juu ya ufahamu wa Salaf. Watu hawa, ambao ni wanachuoni wa falsafa waliokuja baadaye au wanachuoni wa falsafa wa zamani, wote hawa wanahukumu kwa mujibu wa akili yao. Lau akili yao ingelikuwa inategemea Qur-aan na Sunnah tu, na si kama kundi lile la kwanza ambalo linategemea Qur-aan na Sunnah na juu ya ufahamu wa Salaf-us-Swaalih. Sijui kama kunahitajia kwangu kusimama hapa kidogo ili niweze kuonyesha tofauti kati ya watu hawa wawili; wa kwanza yule ambaye anategemea Qur-aan na Sunnah na juu ya ufahamu wa Salaf-us-Swaalih na wa pili anategemea Qur-aan na Sunnah pasi na kurudisha kichwa chake, akili yake na ufahamu wake kwa yale ambayo wema wetu waliotangulia walikuwemo juu yake. Pengine haya hayahitajii ufafanuzi wowote au yanahitajia. Ikiwa mgawanyo huu uko wazi kwa ndugu zetu waliohudhuria na dada zetu pia waliohudhuria, hivyo basi ninasema:

Falsafa hii tunaijua tangu hapo kitambo wakati wanajitegemeza *juu ya maneno*, na sisemi *juu ya akili,* kwa mujibu wa maelezo yaliyotangulia, isipokuwa kwa mujibu *wa akili yao* tu. Wanachotaka ni kumtakasa Allaah na mahali, wakati Yeye Ametakasika na pahali. Kwa mujibu wa Maneno ya Allaah (´Azza wa Jall):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye – Naye ni Mwenye kusikia yote, Mwenye kuona.”[4]

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ

“Wala hawazunguki kitu chochote kile katika Elimu Yake isipokuwa

[4] 42:11

kwa Alitakalo."[5]

[5] 02:255

Maneno ya haki yanayokusudiwa ndani yake batili

Pasi na kujali ni kundi lipi la Kiislamu ambalo mtu yukoemo, kila mtu ni mwenye kuamini kuwa Allaah (´Azza wa Jall) Alikuwepo na hapakuwepo kitu chochote pamoja Naye, kama tunavyojua sisi sote. Hapakuwepo zama wala mahali. Kisha baadaye Allaah (´Azza wa Jall) Akaumba zama na mahali. Kwa ajili hiyo, hakuna shaka yoyote ya kwamba Allaah (´Azza wa Jall) Hayuko katika mahali. Kitu ambacho mtu anatakiwa kukitilia umakinifu ni kuwa, maneno ya huyu Habashiy, ikiwa ni sahihi kusema hivo, tunapata kubainikiwa kutokana na maneno haya kuwa ni neno la haki ambalo ndani yake kumekusudiwa batili, bi maana maneno yao:

”Mahali pameumbwa na ni jambo lisiloingia akilini Allaah Akawa ndani katika kitu kilichoumbwa.”

Maneno haya ni kweli, lakini pamoja na hivyo ni neno la haki ambalo ndani yake kunakusudiwa batili. Ni batili ipi ambayo inakusudiwa kwa neno hili? Wanachokusudia ni kumkanushia Allaah (´Azza wa Jall) Sifa na Majina Yake ambayo Amejisifia nayo (Tabaarak wa Ta´ala) katika Qur-aan na Sunnah ambazo ni Swahiyh. Sisi tunakubaliana nao ya kwamba Allaah (´Azza wa Jall) Hayuko katika sehemu, lakini wao wanakubaliana na sisi kwa yale ambayo Allaah (´Azza wa Jall) Amesema:

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ

“Mwingi wa huruma amelingana juu ya ´Arshi.”?[6]

Wanasema pamoja na sisi kama ilivyo katika Aayah Tukufu:

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ

”Kwake pekee ndiko linapanda neno zuri na kitendo chema Hukipa hadhi.”?[7]

Wanasema pamoja na sisi, kama jinsi Alivyosema Mola Wetu:

[6] 20:05

[7] 35:10

تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ

“Malaika na Roho wanapanda juu Kwake katika siku kiasi chake ni miaka khamsini elfu.”?[8]

Je, wao wanasema kama jinsi tunavyosema? Kwa masikitiko makubwa jibu ni hapana. Kwa ajili hiyo, ni neno la haki ambalo ndani yake kunakusudiwa batili. Hivi sasa itakuja kuwabainikia na kila mmoja mwenye kusikia utatizi wa Ahbaash hawa. Tunasema ya kwamba (´Azza wa Jall) Amejisifu Mwenyewe katika Aayah hizi na nyenginezo na katika Hadiyth ambazo ni nyingi sana ya kwamba Ana Sifa ya ´*Uluw* (kuwa juu), ya kwamba (Tabaarak wa Ta´ala) Ana Sifa ya kuwa juu. Ni jambo lisilokuwa na shaka yoyote kuwa mwenye kuswali wakati anaposujudu husema:

”Subhaana Rabbi al-A´laa” (Kutakasika ni Kwako Allaah, uliye juu)

Vilevile miongoni mwa adabu za kisomo katika Qiyaam-ul-Layl katika Swalah ya usiku imamu anaposoma:

”Sabbih isma Rabbikal-A´laa” *(Sabihi Jina la Mola wako, Aliye juu)*

maamuma nyuma yake waseme:

”Subhaana Rabbi al-A´laa” *(Kutakasika ni kwa Mola wangu, Aliye juu*)

na mfano wa hayo katika maandiko mengi katika Qur-aan na Sunnah ambayo ni dalili zenye kukata kabisa zinazoonyesha ya kwamba Allaah (´Azza wa Jall) ana Sifa ya kuwa juu ya viumbe wote.

Je, wao ni wenye kusema kwa msemo wao kuwa Allaah Hayuko mahali, ya kwamba Allaah Amelingana juu ya ´Arshi Yake? Hawasemi hivo. Sababu inaweza kuwa moja kati ya mambo mawili na lile ambalo husemwa:

“Tamu katika hayo ni chungu.”

Ima inatokana na upotevu wa kifikira na akili, bali na kasoro katika akili na fahamu, au ima ni makusudio ya kuubomoa Uislamu kuanzia upande wake ulio na nguvu zaidi, bi maana ni ´Aqiydah iliyo na mafungamano na Allaah (Tabaarak wa Ta´ala). Kama jinsi

[8] 70:04

mmevyojua tamu katika hayo ni chungu. Ni mamoja ikiwa msemo wao huu ni kutaka kukanusha yale Aliyoyaweka wazi Allaah (´Azza wa Jall) katika Aayah hizi na maandiko ambayo tumetaja na ambayo hatukuyataja, ya kwamba Allaah Ana Sifa ya kuwa juu. Ukanushaji wao wa Sifa hii ima ikawa unatokana na kasoro katika akili, fahamu na elimu au ikawa ni njama dhidi ya Uislamu na Waislamu. Tamu katika hayo ni chungu.

Tunasema hivi sasa kwamba Allaah Hayuko katika mahali ambapo Amepaumba baada ya kutokuwepo kwake. Huu ni uhakika usiokuwa na shaka yoyote ndani yake. Lakini, je, Allaah (´Azza wa Jall) Yuko juu ya viumbe wote pasi na kuwepo katika mahali? Hakuna mafungamano yoyote kati ya hayo mawili, na hapa kunadhihiri ujinga wa watu hawa au njama zao. Hakuna mafungamano yoyote kabisa kati ya kuthibitisha Sifa ya kuwa juu kwa Allaah (´Azza wa Jall) ya viumbe wote na kati ya Yeye kuwa katika mahali. Kwa sababu linaposemwa neno "mahali" kunakusudiwa kitu ambacho hapo kabla hakikuwepo kisha baadaye Allaah (´Azza wa Jall) Akakiumba. Kwa hivyo, wale ambao wanaanza maneno yao kwa falsafa:

"Je, mahali pameumbwa au hapakuumbwa?"

Ndio, pameumbwa.

"Je, inamstahikia Allaah ambaye ndiye Ameumba mahali awe katika mahali hapo?"

Jibu ni kwamba haistahiki.

"Hivyo basi, vipi mtu anaweza kusema kuwa Allaah Yuko katika mahali"?

Makundi mawili yanayomnasibishia Allaah kuwa na mahali

Tunasema:

Hakuna Muislamu yeyote anayesema kuwa Allaah Yuko katika mahali, isipokuwa waliopotea katika Qur-aan na Sunnah. Kuna makundi mawili, kundi limoja linamthibitishia Allaah mahali na huenda mmesikia uthibitisho huu kutoka kwa wale ambao wanajinasibisha na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah katika sisi. Hatuhitajii kuwapeleka mbali. Mara nyingi mmoja wetu katika baadhi ya vikao anasikia kwa masikio yake Muislamu akisema – na sio katika Ahbaash – mara nyingi tunasikia wakisema:

"Allaah Yuko kila mahali."

"Allaah Yupo katika kila kiumbe."

Hii ´Aqiydah sio katika ´Aqiydah ya Waislamu kabisa. Hii ni ´Aqiydah ya moja katika makundi mawili yaliyopotea katika ´Aqiydah sahihi ambayo tumeitaja punde tu ya kwamba Allaah (´Azza wa Jall) Amelingana juu ya ´Arshi. Mu´tazilah wa zamani na wa sasa. Mu´tazilah wa zamani wanasema wazi kabisa ya kwamba Allaah Yuko kila mahali. Kundi jengine leo ambalo halijulikani kwa jina la "Mu´tazilah", lakini linajulikana kwa jina jengine. Kundi ambalo ni kundi miongoni mwa makundi ya Khawaarij na sisi sote tunajua kitu kidogo katika historia yao na upotevu wao wa mambo mengi katika ´Aqiydah sahihi. Kundi hilo liliyopo leo ni lenye kujulikana kama Ibaadhiyyah. Ibaadhiyyah leo wana ´Aqiydah ya Mu´tazilah, ya kwamba Allaah Yuko kila mahali.

Hivi sasa hatutozungumzia kuhusu watu hawa, kwa kuwa mnajua kuwa ni wenye kukosea pale ambapo wanampachika Allaah (´Azza wa Jall) kuwa kila mahali. Lakini kwa masikitiko makubwa mnatakiwa kutilia makini na kukumbuka ya kwamba hawa Ahbaash na watu mfano wao, wakati wanapokutana na baadhi ya Waislamu wa kiume na wa kike na kuwafanya kuwa na mashaka juu ya ´Aqiydah yao sahihi, amabyo ni Allaah (´Azza wa Jall) Amelingana juu ya ´Arshi, namna gani? Hili ni jambo ambalo mtu hawezi kuuliza kama mnavyojua, na hii ni mada nyingine.

Badala ya kusahihisha yale ambayo leo tunayasikia katika vikao vya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, kwamba Allaah Yuko kila mahali, badala ya kusahihisha kosa hili, wanasahihisha ´Aqiydah ambayo ni sahihi na kulingania hilo ili kusahihisha kosa hili. Mu´tazilah wa zamani na wale waliokuja baadaye Ibaadhiyyah, wanasema waziwazi kuwa Allaah Yuko kila mahali, jambo ambalo ni upotevu uliokuwa mkubwa.

Tunaweza kusimama kidogo ili kufafanua kidogo kuhusu upotevu huu. Kuhusiana na kundi la pili ni wale ambao wanasema Allaah Hayuko katika mahali popote kabisa, sawa ikiwa ni mahali ambapo pamepatikana – yaani hapa ni mahali ambapo kulikuwa hapakuwepo kisha Allaah Akapaumba baadaye – au mahali palipoumbwa. Sote tunajua, kama nilivyowatajia mwanzoni, kwamba Allaah (´Azza wa Jall) Alikuwepo na hapakuwepo zama wala mahali.

Je, Alikuwepo katika mahali?

Ikiwa makusudio ya mahali ni mahali palipoumbwa, jibu ni hapana!

Alikuwepo na hapakuwepo kitu chochote pamoja Naye. Lakini Alikuwepo na Alikuwepo katika mahali. Ikiwa kwa neno "mahali" mtu anakusudia mahali palipoumbwa, jibu ni hapana. Lakini Alikuwepo katika mahali ambapo hapakuwepo ambapo baadaye Amepaumba na Akafanya sehemu iliyoumbwa kwa kusema: *"Kuwa!"* na kukawa. Allaah Alikuwepo na hapa panapokusudiwa bado Yuko kama jinsi Alivyokuwa, bi maana Hayuko katika mahali ambapo kumeumbwa. Hili ni jambo liko wazi sana.

Kundi la pili linapinga Allaah kuwa kama jinsi Alivyokuwa milele, bi maana hakuwepo mahali. Kwa ajili hiyo wao hawamthibitishii Sifa ya kuwa juu ya viumbe wote. Watu hawa wana msemo katika misemo ambayo kafiri anaweza kusema na sisemi Muislamu. Hili kundi la pili ambalo linatofautiana na Mu´tazilah katika upotevu wao.

Mnajua kuwa Mu´tazilah wanasema kwamba Allaah Yuko katika kila mahali. Huu ni upotevu wa wazi na hauhitajii maelezo angalau kwa sasa.

Wale ambao wanasema kuwa Allaah Hayuko katika mahali, kama wanavyosema Mu´tazilah na kama wanavyosema Ahbaash, watu hawa hawasemi kuwa Allaah Ana Sifa ya kuwa juu ya viumbe wote, ambayo hakuna yeyote anayejua namna yake isipokuwa Allaah (´Azza wa Jall) pekee.

Wanasema nini?

Wanasema, na usikilize sasa na utilie makini na hii ndio ´Aqiydah ya Ahbaash, na ninamuomba yule anayepata kusikia wasiwasi wao ajue matokeo ya wasiwasi wao, nao ni kukanusha kuwepo kwa Muumba. Ni kukanusha kuwepo kwa Muumba na ni njia inayopelekea katika ukanamungu kikamilifu. Haya ndio madhehebu ya wakomunisti, wakanamungu, mazanadiki na makafiri. Wanasema kuwa hakuna kitu kingine isipokuwa haya hayayoonekana (mazingira).

Sikiliza sasa wanavyomuelezea Mola Wao:

“Wanasema kuwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) Hayuko juu wala chini, kuliani wala kushotoni, mbeleni wala nyumani, ndani ya ulimwengu wala nje ya ulimwengu.”

Sisi tumekubaliana na wao ya kwamba mahali pameumbwa na ni ulimwengu, na Allaah Hayuko ndani ya ulimwengu. Lakini kuhusu kwamba Hayuko nje ya ulimwengu; huu ndio ukanajimungu na ukanushaji wa kikamilifu. Baadhi yao wamepitiliza katika kukanusha na kupinga na wakasema baada ya kusema “Hayuko ndani ya ulimwengu wala nje yake”, hivyo wakawa wamesema:

“Hakufungamana nao wala hakuachana nao.”

Huu ndio ukanushaji na ndio yanayosemwa na wakanamungu wote. Napendelea katika mnasaba huu kuzungumzia majadiliano yaliyotokea baina ya Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) na ajaze kheri Uislamu na Waislamu na baina ya wanachuoni wa falsafa, kama mfano wa hawa Ahbaash. Walikuwa wamemshtaki Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah kwa kiongozi wa nchi siku moja Demeski**,** kwa sababu amesema kadhaa na kadhaa na eti anamfanya Allaah kuwa na kiwiliwili na wakamtuhumu kwa mambo ambayo alikuwa hana. Wakaomba kama kunaweza kupangwa mkutano ili waweze kujadiliana naye. Amiri akakubali hilo na akamwita Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah na wapinzani wake. Wakakaa mbele ya amiri. Amiri akawa amesikia madai ya mashaykh hawa na akasikia kwa Shaykh-ul-Islaam Aayaat na Ahaadiyth ambazo zinamthibitishia Allaah (´Azza wa Jall) kuwa Yuko juu ya viumbe Wake, pamoja na matakaso kamilifu, kama jinsi imevyowekwa wazi katika Qur-aan:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye – Naye ni Mwenye kusikia yote, Mwenye kuona.”[9]

Wakati aliposikia maneno ya Shaykh kwa upande mmoja na maneno ya wanachuoni hawa kutoka upande mwingine akasema - na hili linaonyesha akili na hekima ya hali ya juu - akasema:

“Hawa ni watu ambao wamempoteza Mola Wao.”

[9] 42:11

Haya ni maneno ya kweli. Watu ambao wanasema kuhusu Mola Wao kwa kifupi, kwa kuwa hakuna haja ya kukariri yaliyosemwa. Inatosheleza kukumbuka matokeo:

"Hayuko ndani ya ulimwengu wala nje ya ulimwengu. Hakufungamana nao wala hakuachana nao."

Amiri yule amesema kweli pindi aliposema kuhusu watu hawa:

"Hawa ni watu ambao wamempoteza Mola Wao."

Ikiwa tutasema kumwambia mtu ambaye ni mfaswaha mzuri wa lugha ya kiarabu atuelezee kitu kisichokuwepo, basi hawezi akatuelezea kwa njia bora zaidi kama jinsi watu hawa wamevyomuelezea Mola Wao.

Kitu kisichokuwepo ni kile ambacho hakipo ndani ya ulimwengu wala nje yake. Allaah ni namna hiyo? Hapana.

Allaah Alikuwepo na hapakuwepo kitu pamoja Naye. Kwa ajili hiyo amesema Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah wakati alipokuwa anaelezea kuhusu makundi yote mawili, *Mujassimah* ambao wanamshabihisha Allaah na baadhi ya viumbe Wake, wale ambao Ahbaash hawa wanajificha nyuma yao, wanakanusha kwa Allaah kuwa na mfano wa Sifa ya Mikono ambayo Ameitaja katika Qur-aan na Sifa zengine ambazo tutazitaja karibuni – in shaa Allaah. Ibn Taymiyyah amewasifu watu hawa *Mujassimah* kwa sifa nzito sana, kama jinsi vilevile amewasifu *Mu´attwilah*. Amelinganisha makundi haya mawili na akawakusanya katika sifa ambayo wanakusanyikiwa na upotevu. Amesema:

"*Mujassimah* anaabudu sanamu na *Mu´attwilah* anaabudu kitu kisichokuwepo."

Huu ndio ukweli. *Mujassimah* anaabudu sanamu. Allaah Hana kiwiliwili, Ametakasika Allaah. Hakuna chochote kinachofanana Naye, Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

Kuhusiana na *Mu´attwilah* anaabudu kitu kisichokuwepo. Kivipi?

"Hayuko ndani ya ulimwengu wala nje ya ulimwengu. Hakufungamana nao wala hakuachana nao."

Hii ndio ´Aqiydah ya Mu´tazilah na wanachuoni wa falsafa na miongoni mwao wanaingia pia Ashaa´irah hii leo na baadhi ya Maaturiydiyyah hapo zamani. Hata kama Maaturiydiyyah wengi hii leo, ambao hawasemi neno la haki, ambalo limesemwa na baadhi ya Maaturiydiyyah waliotangulia ambao walishikamana na uongofu wa Salaf-us-Swaalih. Mmoja wao amesema kwa haki:

“Mola wa ´Arshi Yuko juu ya ´Arshi, bila ya maelezo ya uwezo na mafungamano.”

Allaah (´Azza wa Jall) kama jinsi Alivosema, Amejitosheleza na walimwengu. Allaah (´Azza wa Jall) Amelingana juu ya ´Arshi, bi maana juu ya viumbe wote. Sio kwa sababu ni Mwenye haja nayo, bali ili Aweze kuyaendesha na Kuyasimamia mambo na awe juu ya viumbe Wake wote.

Hapa tunaweza kusema kuwaambia hawa Ahbaash na mfano wao katika wale waliyopotea katika ´Aqiydah ya Salaf-us-Swaalih, ya kwamba Allaah (´Azza wa Jall) Yuko juu ya ´Arshi kwa mujibu wa andiko la Qur-aan tukufu na tafsiri ya Salaf-us-Swaalih.

Nyinyi mnasema kuwa Allaah (´Azza wa Jall) Hayuko katika mahali na mnasema: Je, inajuzu kwa Muislamu kuuliza “Allaah Yuko wapi?”

Hapa pazia inakuja kufichuliwa kwa watu hawa ambao wanajificha kwa kumtakasa Allaah (´Azza wa Jall) kwa kuwepo katika mahali palipoumbwa. Lakini, tunawauliza sasa, je, Allaah (´Azza wa Jall) Yuko mbinguni? Pamoja na kujua kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye ambaye ametuonyesha sisi Waislamu tunaofuata Qur-aan na Sunnah na kwa mfumo wa Salaf-us-Swaalih kumuuliza yule ambaye tuna mashaka juu ya imani yake, ikiwa anamwamini Allaah (´Azza wa Jall):

“Allaah Yuko wapi?”

Na kwa ajili hiyo ikaonyeshwa kwetu jinsi mtu atakavyojibu, jibu ambalo ni:

“Allaah Yuko juu mbinguni.”

Mjakazi – Allaah Yuko wapi?

Lakini hili linahitajia ufafanuzi, bi maana pale tunaposema kuwa Allaah Yuko mbinguni. Nitafanya hivo – in shaa Allaah – baada ya kuwakumbusha ndugu na dada zangu wasikilizaji juu ya Hadiyth iliyopokelewa na maimamu katika vitabu vyao na ambayo wameafikiana kwayo wanachuoni wa Hadiyth, wanachuoni wa Tafsiyr, wanachuoni wane wa Fiqh na wengineo kwamba ni Swahiyh. Imaam Muslim, ambaye ni mmoja katika watu wa Hadiyth, ameipokea katika "as-Swahiyh" yake, kabla yake Imaam Maalik katika kitabu chake "al-Muwattwa´" yake, baada yake Imaam Ahmad katika kitabu chake "al-Musnad" na wengineo ambao ni wengi sana miongoni mwa wale waliowafuata kwa wema.

Hadiyth hiyo imepokelewa kwa mnyororo ambao ni Swahiyh na Mu´aawiyah bin al-Hakam as-Sulamiy (Radhiya Allaahu ´anh) kwamba siku moja aliswali nyuma ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mtu mmoja pembezoni mwake akapiga chafya wakati alipokuwa anaswali na akasema kumwambia:

يرحمك الله

"Allaah akurehemu."

Wakamtazama kwenye ncha ya macho (yaani wale wengine waliokuwa wanaswali) ili kumnyamazisha, lakini inaonekana kuwa ndio alikuwa ameingia katika Uislamu karibuni, mpya juu ya ujuzi wa hukumu zinazohusiana na swalah na ndio maana hakuweza kuwavumilia pindi alipoona wamemtazama mtazamo wa kumnyamazisha. Akasema kwa sauti ya juu:

"Kwa nini mnanitazama?"

Hivyo wakaanza kupiga kwenye mapaja yao na kujaribu kumnyamazisha. Kana kwamba hapo ndipo alipoelewa kuwa amefanya kosa na kutaja uongofu wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) namna alivyofanya naye upole na kusema:

"Wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipokuwa amemaliza swalah akanijia, na ninaapa kwa Allaah kwamba hakunikwaza, hakuniudhi, hakunipiga wala hakunitukana, bali alinambia:

"Hii ni swalah. Si jambo la sawa ndani yake kukawa kitu katika maneno ya watu, kuna Tasbiyh, Takbiyr na Tahmiyd"."

Wakati mtu huyu alipoona upole huu, na ni mtu ambaye amesifiwa na Mola wa walimwengu katika Qur-aan tukufu:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ

”Na hakika wewe bila shaka una tabia nzuri mno.”[10]

Wakati alipoona upole huu katika kumfundisha kwake, akapatwa na hamu ya kujifunza zaidi baada ya kutambua kuwa amefanya kosa katika swalah, pindi alipozungumza na wakati ilikuwa haijuzu kwake kuzungumza. Akasema:

“Ee Mtume wa Allaah! Kati yetu kuna watu ambao wanaamini mikosi.”

Akasema:

“Wasikugeuzeni.”

Akasema:

“Kati yetu kuna watu ambao wanawaendea makuhani.”

Akasema:

“Usiwaendee.”

Akasema:

“Kati yetu kuna watu wanaopiga misitari kwenye udongo.”

Akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Kulikuwepo Mtume miongoni mwa Mitume anayepiga misitari, yule ambaye misitari yake itaafikiana na misitari yake basi inafaa.”

Akasema:

“Ee Mtume wa Allaah – na hapa ndipo kunakuja tunachokikusudia, na yaliyotajwa yanahitajia muhadhara au mihadhara zaidi, lakini nukta muhimu ni hii inayokuja – Akasema: “Ee Mtume wa Allaah! Mimi nina mjakazi anayenichungia kondoo karibu na Uhud. Siku moja mbwamwitu alimchukua kondoo mmoja. Mimi ni mtu ninayeghadhibika

[10] 68:04

kama jinsi wanavyoghadhibika watu wengine, nikampiga kipigo na ninataka kuacha mtumwa huru.” Hivyo akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Mlete.”

Alipokuja Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamuuliza:

“Allaah Yuko wapi?”

Akasema:

“Juu ya mbingu.”

Akamwambia:

“Mimi ni nani?”

Akasema:

“Wewe ni Mtume wa Allaah.”

Hivyo akasema kumwambia yule bwana wake:

“Mwache huru. Kwani hakika ni muumini.”

Hadiyth hii wameafikiana wanachuoni wa Waislamu, kwa fani zao mbalimbali, kama wanachuoni wa Hadiyth, na hii ndio fani yao, wanachuoni wa Tafsiyr, wanachuoni wa Fiqh na wanachuoni wa Tawhiyd, wote wamekubaliana ya kwamba Hadiyth hii ni Swahiyh.

Ambao hawakuafikiana nao tu ni wanachuoni wa falsafa, ambao wanaingiza vichwa vyao na wanafuata matamanio yao. Wao ndio wanairudisha Hadiyth hii kwa kutumia akili zao, akili ambazo mmejua ya kwamba hazina thamani yoyote.

Hadiyth hii imetufanyia kuwa ni Sunnah kwetu kujuzu kuwauliza watu hawa Ahbaash na watu mfano wao katika wafuasi wa Mu´tazilah, Ibaadhiyyah, Allaah Yuko wapi? Utawaona namna wanavyochanganyikiwa. Wanasema kuwa swali hili halijuzu, lakini hawajui kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye ambaye amefanya swali hili kuwa ni Sunnah juu ya Ummah wake. Wanamraddi Mtume wao, ambaye wanadai kuwa wanamwamini.

Kisha jibu la mjakazi ilikuwa:

“Allaah Yuko mbinguni.”

Pengine hamuamini hilo, lakini kitabu kipo. Hakika baadhi ya wanachuoni wa zama hizi wanasema kauli ya kusema kwamba Allaah Yuko juu ya mbingu ni ´Aqiydah kabla ya kuja Uislamu na sio ´Aqiydah ya Waislamu. Ama kuhusu msemo huu, ya kwamba Allaah Yuko juu ya mbingu ndio ambao Ameulezea Mola wa walimwengu katika Qur-aan Tukufu. Kama jinsi mnavyojua katika Suurah Tabaaraka:

أَأَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ أَن يَخْسِفَ بِكُمُ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورُ أَمْ أَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ أَن يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۖ فَسَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ

“Je, mnadhani mko katika amani na Yule Aliyeko mbinguni kwamba Hatokudidimizeni ardhini, tahamaki hiyo inatikisika? Au mnadhani mko katika amani na Yule Aliyeko mbinguni kwamba Hatokutumieni kimbunga, basi mtajua vipi [ni makali] maonyo Yangu?”[11]

Kuna kundi lingine ambalo liko karibu na uongofu na liko mbali na upotevu kuliko kundi lile la kwanza, bi maana lile ambalo linasema kuwa msemo wa kwamba Allaah Yuko juu ya mbingu ni msemo wa kabla ya kuja Uislamu. Wanaifasiri kimakosa Aayah hii kwa taawili ya kusema kwamba aliye mbinguni maana yake ni Malaika. Haya ndio yale wanayoita kuwa ni *Majazi*. Wanatumia *majazi* ili waweze kukanusha Sifa ya Kiungu. Kuna Ahaadiyth nyingi ambazo zinakanusha taawili kama hizi. Miongoni mwa Ahaadiyth hizo ni Hadiyth ambayo imeenea baina ya watu leo, lakini watu wengi hawaijui, bali hawafahamu ni nini wanachokisema. Hadiyth hiyo ni hii ifuatayo:

“Wenye huruma wanahurumiwa na Mwingi wa huruma. Muhurumie aliye juu ya ardhi (fiyl-Ardhw), hivyo Atakuhurumieni aliye juu ya mbingu (fiys-Samaa´).”

Ni nani aliye juu ya mbingu? Ni Allaah. Ni kina nani walio juu ya ardhi? Ni viumbe wa Allaah, kama wanaadamu, wanyama na kadhalika. Kwa vile Hadiyth hii inawekwa wazi maana inayokusudiwa na Kauli Yake (Ta´ala):

أَأَمِنتُم مَّن فِي السَّمَاءِ

[11] 67:16-17

“Je, mnadhani mko katika amani na Yule Aliyeko mbinguni?”

Haya ndiyo yale niliyosema karibuni kwamba huenda tunalazimika kubainisha maana ya “fiys-Samaa´”. Kwa sababu neno “fiy” katika lugha ya kiarabu wakati fulani inakuja kwa maana ya kielezi (Dhwarfiyyah) na wakati mwingine inakuja kwa maana nyingine kama kihusishi (Huruuf-ul-Jarr). Inaweza kuja kama maana ya “juu”. Katika Aayah hii “fiy” ina maana ya kielezi. Jibu ni hapana.

Hapa wanadhani wale wanachuoni wa falsafa ya kwamba wakikanusha Allaah kuwa juu ya mbingu, ya kwamba wamemtakasa. Kwa hakika ni kuwa wamemtakasa kwa ufahamu wao wa kimakosa wa Aayah. Wamepinga kusema kama Alivyosema Allaah, ya kwamba Yuko mbinguni. Hawakufahamu maana ya Allaah kuwa mbinguni, kwamba maana yake yuko juu ya mbingu. Katika hali hii Aayah hii inapata maana ile ile kama Hadiyth iliyotangulia:

“Wenye huruma wanahurumiwa na Mwingi wa huruma. Muhurumie aliye juu ya ardhi (fiyl-Ardhw), hivyo Atakuhurumieni aliye juu ya mbingu (fiys-Samaa´).”

Kinachokusudiwa kwa neno “aliye juu ya ardhi” sio aliye ndani ya ardhi, kama minyoo, wadudu na vyenginevyo, bali maana yake iko wazi kabisa, “aliye juu ya ardhi”, bi maana wale unaotangamana nao katika wanaadamu au wale wanyama ambao Allaah Amewapa. Wahurumieni walioko juu ya ardhi, hivyo atakuhurumieni aliye mbinguni, bi maana yule Aliye juu ya mbingu.

Kwa hiyo, tafsiri hii inawekwa wazi na Hadiyth hii kwa maana hiyo hiyo na Aayaat, ambazo tumezitaja baadhi yake na Ahaadiyth zengine, ambapo Allaah (´Azza wa Jall) Anaelezea kuwa na Sifa ya ujuu.

Wakati tunapowauliza Ahbaash au wengineo ambao wanafanana katika upotevu wao “Allaah Yuko wapi?” Jibu lao linatakiwa kuwa kama alivyojibu mjakazi “Allaah Yuko mbinguni”. Lakini sio kwa ufahamu wake, kielezi “Fiy”, hapana. Bali kwa ufahamu wa kama jinsi ile Hadiyth ya kwanza inavyoweka wazi, na pili kama jinsi Salaf-us-Swaalih wetu walivofuata, Allaah Yuko mbinguni, bi maana juu ya mbingu, bi maana juu ya ´Arshi, kwa sababu kila kilichojuu husemwa kuwa ni mbingu.

Kwa hivyo, mtu anakuwa amewafungia njia zote hawa Ahbaash, ambao kwanza wanaamini kuwa haijuzu kumuuliza Muislamu “Allaah Yuko wapi” na pili wanaamini kuwa haijuzu kusema “Allaah Yuko mbinguni”. Baada ya kuwabainikia ya kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye ambaye amesunisha swali hili, bi maana “Allaah

Yuko wapi?" na ni yeye ndiye ambaye amemshuhudia mjakazi yule kuwa na imani, wakati alipotamka kwa matamshi ya Qur-aan: "Allaah Yuko mbinguni".

Hapa kuna somo ambalo ni lazima nilitaje. Nalo ni kwamba, inapata kutubainikia kwetu tofauti kati ya maisha ambayo jumla ya Waislamu walikuwa wanaishi ndani yake katika zama za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), akiwemo mjakazi aliyekuwa akichunga kondoo, na kati ya maisha ambayo jumla ya Waislamu na wengi katika wale wasomi wao wanaishi hii leo. Kwa kuwa swali hili lau utawauliza nalo wengi katika wale wasomi, na kati yao wamo wale wanachuoni wakubwa wa Azhar, ambayo inaelezwa kwa Azhar Tukufu. Lau mtu atawauliza swali hili "Allaah Yuko wapi?", hawatojibu kwa jibu la mjakazi. Iko wapi tofauti kati ya hao wanachuoni wakubwa katika zama zetu, wasiojibu kwa swali la Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kati ya mjakazi mchunga kondoo ambaye alijua jibu sahihi juu ya swali hili.

Ninasema: hii ni dalili ya kwamba Waislamu katika wakati ule wa kwanza wote walikuwa wamelelewa, pasi na tofauti yoyote kati ya wale wasomi wao na wale wengine wa kawaida. Wote walikuwa wamelelewa kwa malezi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Angalau kwa uchache na yale yanayohusiana na ´Aqiydah, ambayo ni wajibu kwa kila Muislamu kuifahamu kwanza kisha baadaye aiamini.

Mjakazi huyu vipi alitambua ´Aqiydah sahihi? Jibu ni kwamba, mjakazi huyu hatuwezi kujifikiria kuwa alikuwa anaweza kuhudhuria vikao vya kielimu ambavyo vilikuwa vinahudhuriwa na Maswahabah wakubwa wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wale wasomi wao ilihali wengine walikuwa hawadhuhurii vikao hivi vya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Ikiwa ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh) wakati alipofikiwa na Hadiyth kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) alijutia na kusema "Tulikuwa tumeshughulishwa na mambo ya biashara kwenye masoko". Ikiwa huyu ni ´Umar, tusemeje juu ya wale Maswahabah wengine na tusemeje juu ya wanawake na mwishowe tusemeje juu ya wajakazi na wachunga kondoo.

Ninachokusudia kwa haya ni vipi mjakazi huyu alifahamu ´Aqiydah hii sahihi ambayo mpaka hivi sasa haijafahamika na baadhi ya wale wasomi katika wanawachuoni. Alikuwa akiishi katika mazingira ambayo yalikuwa na umoja katika ´Aqiydah sahihi, yanayokosa mfano duniani, kwa sababu ya kuwepo kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kwa sababu ya mwanga uliokuwepo kati ya Maswahabah, katika wanawaume na wanawake, miongoni mwa wale wasomi na watu wa kawaida.

Mjakazi huyu alichukua ´Aqiydah hii kutoka kwa bwana wake. Bwana wake anasikia ´Aqiydah sahihi, hukumu za Kishari´ah, kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), lakini hatosheki na kubaki nayo mwenyewe, bali anaieneza kwa yule anayemlisha, yule anayemlipa mshahara na elimu. Hapa tunapata kujua ni vipi mjakazi huyu alipata kujua ´Aqiydah hii sahihi. Ni kwa sababu aliishi katika mazingira yaliyokuwa na umoja katika kuifahamu ´Aqiydah sahihi.

Lakini leo Waislamu wanaishi kwa ´Aqiydah zinazotofautiana na kugawanyika katika mgawanyiko mkubwa. Kwa ajili hiyo hakuna njia nyingine ya uokozi kwa Waislamu katika zama hizi, isipokuwa ikiwa kama watarejea kwa yale waliyokuwemo Salaf-us-Swaalih na wahakikishe katika nafsi zao khabari za Mtume wao (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wakati alipoelezea juu ya kundi lililookoka kwa kusema:

“Ni lile ambalo litakuwa juu ya yale niliyomo mimi hivi leo na Maswahabah zangu.”

Mkono wa Allaah

Ninataka kukhitimisha maneno kwa Hadiyth hii, lakini nimekumbuka kwamba lilikuwa katika swali lililoulizwa, ya kwamba miongoni mwa mambo ambayo wanapinga Ahbaash hawa ni Mkono, ambao Allaah (´Azza wa Jall) Amejisifu Mwenyewe. Wanasema kuwa Mkono ni kiungo. Ametakasika Allaah. Wanazungumza wao wenyewe. Vipi, kwa Mkono ambao Allaah Ameutaja, wanaweza kusema kuwa ni kiungo?

Watu hawa ni katika wajinga kabisa wa watu, ikiwa sio katika wapotevu kabisa wa watu.

Hilo kwa kuwa wanalinganisha kisichokuwepo na kilichopo. Bali wanalinganisha kisichoonekana kabisa, ambaye ni Allaah (Tabaarak wa Ta´ala), na wao wenyewe.

Huu ni upumbavu wa kupindukia, ikiwa sio upotevu wa kupindukia.

Tunajiweka katika upande wao na kujadili, na sio katika ´Aqiydah. Allaah Asijaalie tukashirikiana nao katika ´Aqiydah yao.

Tunawaambia:

"Allaah ni Yule ambaye Anasifika kwa Sifa kamilifu", je, nyinyi mnasema kama sisi?

Ni lazima waitikie kwa kusema:

"Ndio, tunakubaliana nanyi au waseme "Hapana". Wakisema "Hapana", basi hilo ndio linaonyesha upotevu wao na kuhakikisha kile wanachoamini. Katika hali hiyo hatuna cha kuzungumza nao, kwa kuwa itakuwa ni kuzungumza na mazanadiki. Kinachotakikana kwa sasa ni sisi kuzungumza na Waislamu wanaoshuhudia ya kwamba hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, wanaswali na mengineyo.

Wakisema "Sisi tunakubaliana na nyinyi ya kwamba Allaah (´Azza wa Jall) Amepwekeka katika Sifa zote za ukamilifu". Wakisema hivi watakuwa wamejigonga wao wenyewe pindi wanaposema kuwa Allaah Amepwekeka na Ana Sifa.

Wewe, unayezungumza kwa maneno ya wanachuoni wa falsafa; wakati unaposema kuwa Mkono ni kiungo, je, kiungo hichi kina uhusiano na dhati yako?

Je, dhati yako ni kama Dhati ya Allaah, au Dhati ya Allaah ni kama dhati yako?

Utasema “Hapana”. Dhati Yake sio kama dhati nyenginezo na kwa ajili hiyo Sifa Zake sio kama sifa za viumbe wengine.

Wapendwa wasikilizaji! Hapo tatizo litakuwa limekwisha. Mtu anasema juu ya Dhati Yake yale anayosema juu ya Sifa Zake. Mtu anasema juu ya Sifa yale anayosema juu ya Dhati. Dhati ya Allaah ina Sifa zote kamilifu na Ametakasika na sifa zote zenye mapungufu. Hiyo ndio maana ya Kauli Yake (Ta´ala):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye – Naye ni Mwenye kusikia yote, Mwenye kuona.”[12]

Yeye ndiye Mwenye kusikia na mwenye kuona kila kitu. Allaah Amezungumza ukweli, lakini Usikizi Wake sio kama usikizi wetu na Uoni Wake sio kama uoni wetu.

Hawa ambao wanajadili kwa batili na wanajificha nyuma ya maneno ya haki – uinje wake ni haki wakati undani wake ni batili – ni lazima wazikanushe Sifa zote za Allaah (´Azza wa Jall). Kwa nini?

Kwa kuwa wakati mtu Anapomsifia Allaah kwa Sifa hizi, mara nyingi kuna kufanana katika matamshi, lakini katika uhakika wa maana sio sawa. Allaah (´Azza wa Jall) Amesema kuhusu Aadam:

فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا

“Tukamjaalia mwenye kusikia na kuona.”[13]

na Amejisifia Mwenyewe ya kwamba ni Mwenye kusikia yote (as-Samiy´), Mwenye kuona yote **(**al-Baswiyr). Kwa ajili hiyo tunamalizia maneno haya kwa kusema:

Ikiwa Allaah Anasema kuwa ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona na amemsifu Aadam (´alayhis-Salaam) kuwa Amemfanya ni mwenye kusikia na kuona. Mtu akifuata njia ya

[12] 42:11

[13] 76:02)

Ahbaash hawa na mfano wao katika Mu´ttwilah (wakanushaji), ni lazima kuwepo mambo mawili.

Ima Allaah awe si kama Alivyosema: "Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona", kwa kuwa haya pia yamesemwa juu ya Aadam: "Tukamjaalia mwenye kusikia na kuona",

au tuseme "Hapana, Yeye ni kama jinsi Alivyojisifu Mwenyewe", lakini Maneno Yake juu ya Aadam **"**Tukamjaalia mwenye kusikia na kuona" sio kama Yeye.

Ni lazima kukanusha moja ya hizo sifa mbili. Ima hiyo inayohusiana na Allaah (´Azza wa Jall), na hii ni kufuru, au hiyo ambayo inahusiana na Allaah kumsifu Aadam (´alayhis-Salaam), kwamba Amemjaalia kuwa mwenye kusikia na kuona, kupinga hili pia ni kufuru. Kwa ajili hiyo, wanazunguka baina ya kufuru na kufuru. Hayo ndio matokeo kwa yule asiyewafuata Salaf-us-Swaalih na kwa ajili hiyo imesemwa:

"Kila kheri inapatikana kwa kuwafuata waliotangulia (Salaf). Kila shari inapatikana kwa kuwafuata waliokuja baadaye (Khalaf)."

Tunawanasihi waliodhuhuria wote wasiwasikilize wanachuoni wa falsafa wala wafuasi wao. Ni lazima kwao wajifunze ´Aqiydah ya Salaf ili wawe – in shaa Allaah – ni wenye kuongoka. Himdi zote ni Zake Mola wa walimwengu.